

## HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



SHULE YA SEKONDARI ZIWA NGOSI,  
S. L. P. 59,  
**TUKUYU.**  
7/12/2020.

Kumb. Na. ZNSS/S.4252/ADM/VOL. 1/09

JINA LA MWANAFUNZI,

.....  
.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ZIWA NGOSI WILAYA YA RUNGWE  
MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.**

**1.0 UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Ziwa Ngosi ipo umbali wa km 32 kutoka mji mkuu wa Wilaya ya Rungwe – Tukuyu na ipo kaskazini mwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Usafiri wa basi kutoka Tukuyu mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Kiwira-Tukuyu.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**2.1 Sare za shule:**

- i) **Wavulana:- Suruali mbili (2)** moja rangi ya damu ya mzee na moja rangi ya kaki. **Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi** ambayo ni tetroni. **Viatu vya ngozi vyeusi** vya kamba jozi mbili vyenye visigino vifupi (viatu vya plastiki haviruhusiwi). **Soksi nyeusi jozi mbili. T-shirt** moja rangi ya kijivu. **Truck suit** moja rangi ya dark blue, **raba** kwa ajili ya michezo. **Sweta moja** rangi ya kijani, **mkanda mmoja wa ngozi** rangi nyeusi.
- ii) **Wasichana:- Sketi mbili (2)** moja rangi ya damu ya mzee na moja ya kaki zenye marinda ya kupanga au kufukuzana na ziwe ndefu zenye kuvuka magoti kwenda chini. Rangi ya hijabu ni nyeupe. **Mashati mawili meupe mikono mifupi** ambayo ni tetroni. **Viatu vya ngozi vyeusi** vya kamba jozi mbili vyenye visigino vifupi (viatu vya plastiki haviruhusiwi). **Soksi nyeupe** ndefu jozi mbili. **T-shirt moja** rangi ya kijivu. **Truck suit** moja rangi ya dark blue, **raba** kwa ajili ya michezo. **Sweta moja** rangi ya kijani.

**2.2 VIFAA VYA DARASANI:**

- i) Madaftari 9 makubwa – counter book (quire 2).
- ii) Mkebe 1, biki, penseli na rula.
- iii) Kamusi ya Kiswahili – Kiingereza.
- iv) Begi imara la kubebea daftari.
- v) Faili moja la kamba (folder file).
- vi) Picha ndogo (2) za passport size kwa ajili ya jalada na kuweka ubaoni.

**2.3 VIFAA VYA USAFI:**

- i) Mfagio mmoja (chelewa).
- ii) Jembe na mpini.
- iii) Ndoo ya lita 10 kwa ajili ya maji.

#### 2.4 CHAKULA:

Zingatia waraka wa Elimu namba 6 wa mwaka 2015 kuhusu utekelezaji wa Elimu msingi bila malipo wenye Kumb. Na. **ED/OKE/NE/VOL. 11/01/61 kipengele/kifungu 3.6 (i)**.

“Wazazi/walezi watendelea kufanya yafuatayo:-

Kununua sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia vikiwemo:- madaftari na kalamu na chakula kwa wanafunzi wa kutwa.

Wazazi wa wanafunzi wa shule hii watakubaliana namna ya kuhakikisha watoto wao wanapata chakula cha mchana wawapo shuleni kama ilivyopendekezwa na Halamshauri ya Wilaya ya Rungwe.

#### 3.0 MAADILI MEMA:

- A. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na wanafunzi wengine kwa ujumla ni jambo la lazima.
- B. Utatakiwa kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- C. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- D. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
- E. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- F. Kufahamu na kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

#### 4.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE:-

- i) Wizi.
- ii) Uasherati, ubakaji na ushoga.
- iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- iv) Uvutaji bangi na sigara.
- v) Makosa ya jinai.
- vi) Kupiga au kupiga.
- vii) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma na ya mwenzako.
- viii) Kudharau Bendera ya Taifa, wimbo wa taifa, fedha za taifa.
- ix) Kuo au kuolewa.
- x) Kupata mimba au kusababisha au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- xi) Kutoa mamba.
- xii) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- xiii) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- xiv) Utoro.
- xv) Kupatikana na simu ya mkononi.

#### 5.0 MAMBO YA MENGINE MUHIMU:

Utatakiwa kuwa na fomu zifuatazo zikiwa zimejazwa kikamilifu:-

- A. Fomu ya uchunguzi wa daktari (Medical Examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- B. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- C. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- D. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

6.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI ZIWA NGOSI.**

.....  
**GEOFREY K. MGINA**  
**MKUU WA SHULE**  
**0755 078 382**